"MKOA WA ARUSHA"
Baruazoteziandikwekwa:
Mkuuwashule
ShuleyaSekondariOldonyolengai,
Simu Na. +255 784758601
+255 735758601
E-Mail Address: headmasteroldonyolengai@gmail.com

OLDONYO LENGAI SEKONDARI
S. L. P 26,
MTO WA MBU,
ARUSHA.

Kumb Na. OLSS/F.I/SELECTION/2024.Tarehe: _____

JINA LA MZAZI/MLEZI: _____,

S. L. P. _____,

Ndugu;

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI OLDONYO LENGAI KWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024.

1.0: UTANGULIZI.
Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2024**. Shule ya sekondari oldonyo lengai ipo umbali wa kilometa **56** kaskazini mwa mji wa Mto wa mbu, kata ya Engaruka, Tarafa ya Manyara halmashauri ya Wilaya ya Monduli. usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi cha Arusha kwa nauli ya **10,000**/= na nauli ya **6,000/=** kutoka kituo cha mji wa Mto wa mbu hadi Engaruka/kibao cha shule yetu.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia siku ya Jumamosi, Januari **06.2024** hadi kufikia Jumatatu, Januari **22, 2024**. mara baada ya tarehe hiyo ya mwisho, mwanafunzi asiporipoti shuleni, mzazi/mlezi atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu.

Aidha, iwapo utampeleka mwanao shule binafsi, toa taarifa mapema kwa mkuu wa shule au kwa Afisa elimu sekondari kuepuka usumbufu wa kukamatwa.

1.1: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.
1.1.0: SARE ZA SHULE.
A: WAVULANA.

1. Suruali za rangi ya maroon (**damu ya mzee** kitambaa namba moja) jozi 2 zenye upana wa nchi 16 chini yenye pindo(turn up)
2. Shati jeupe mikono mifupi jozi 2;
3. soksi nyeusi jozi 2;
4. Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na soli fupi jozi 2;
5. Suruali za rangi ya **khak**i kitambaa namba moja kwa ajili ya kuvaa baada ya muda wa madarasani/shamba dress jozi 2;
6. T-shirt za maroon/**damu ya mzee** jozi 2 kwa ajili ya kuvaa baada ya madarasani na isiyo na maandishi yoyote;
7. Mkanda mweusi wa suruali wenye bakoli ndogo
8. Sweta la maroon (**damu ya mzee**) yenye shingo V

SARE ZA MICHEZO KWA WAVULANA

1. T- shirt na bukta jezi ya **maroon**
2. Track suit rangi ya **Maroon**
3. Raba za michezo

B: WASICHANA.

1. Sketi za rangi ya maroon (**damu ya mzee** kitambaa namba moja) zinazovuka magoti zenye marinda ya kawaida jozi 2; Kwa wale wanafunzi wa kiislamu waje na sketi ndefu za rangi na mashono yaliyotajwa.
2. Shati jeupe mikono mifupi jozi 2; kwa wasio waislamu
3. Half kanzu (nusu kanzu) kwa waislamu jozi 2 nyeupe
4. Soksi nyeupe za kufika chini kidogo ya magoti jozi 2;
5. Viatu vyeusi vya ngozi, kamba na soli fupi jozi 2;
6. Sketi za rangi ya **khak**i(kitambaa namba moja) kwa ajili ya kuvaa baada ya muda wa kawaida wa madarasani jozi 2(shamba dress);
7. T-shirt ya maroon(**damu ya mzee** kitambaa namba moja) jozi 2 kwa ajili ya kuvaa baada ya muda wa kawaida wa madarasani isiyo na maandishi yoyote;
8. Awe na sweta la maroon (**damu ya mzee**) yenye v shingoni;
9. Hijabu jozi 2 au zaidi na iwe ni rangi nyeupe ifanane na nusu kanzu ya shule.

1.1.1: SARE ZA MICHEZO.

1. T-shirt na bukta ya jezi ya **maroon**
2. Tracksuit ya **maroon**
3. Raba za michezo jozi 1.

1.2: MAHITAJI MENGINEYO.

1. Daftari kubwa (counter book quire three (q3)) tisa (9), mkebe/kofa,rula,ufuto,penseli na kalamu za kutosha;
1. Nauli ya kwenda likizo ambazo zitahifadhiwa kwa mhasibu. pia mwenye bima za afya kama CHIF/NHIF aje nayo na itatunzwa kwa mwalimu wa afya; ambaye hana bima ya afya aje na shilingi elfu sita (6000 kwa ajili ya bima).
2. Aje na sabuni za kufulia/kuogea, dawa ya meno na mswaki, taulo ya kuogea, malapa, kitana ,saa,taulo za kike, nguo za ndani za kutosha, tochi, rangi ya viatu, mafuta ya kupaka,brashi ya kupakia rangi na brashi ya kung'arisha viatu
3. Godoro la upana wa futi $2\frac{1}{2}$, unene wa inchi 3 liwe TANFOAM iliyoshonewa foronya;
4. Shuka mbili za rangi ya bluu kwa wasichana
5. Shuka mbili za rangi ya pink kwa wavulana;
6. Ndoo 2 za plastiki ya lita 10 kwa ajili ya kuogea/kufulia;
7. Sanduku imara la bati lenye kufunga sehemu mbili na kufuli zake;
8. Chandarua ya mbu ya pembe nne;
9. Mzazi/mlezi ahakikishe analeta fomu yetu hii ya kujiunga na kidato cha kwanza siku ya kumripotisha mtoto
10. Aje na vyombo vya chakula kama sahani, bakuli, kikombe (vyote vya mifupa) na kijiko.
11. Aje na **jembe** kwa ajili ya usafi na **Rim paper moja**(plain/isiyo na mistari)
12. Mzazi ahakikishe anakuja na fomu ya daktari iliyojazwa katika hospitali ya Serikali yenye Mhuri.
13. Ni lazima Aje na **kamusi ya '*Kiswahili sanifu'*** pia aje na '***Dictionary ya English to English'***



SHERIA NA KANUNI MUHIMU
SHULE YA SEKONDARI OLDONYO LENGAI

1.0: HESHIMA.

1. mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano;
2. mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yake na mwanafunzi mwenzake, mwalimu na watu wengine;
3. mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kwake kama wazazi wake;
4. mwanafunzi anatakiwa kushirikiana na wanafunzi wenzake katika kazi;
5. mwanafunzi haruhusiwi mkufanya mambo yafuatayo:-
    - kumiliki simu;
    - kufuga kucha ndefu na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi;
    - kufuga ndevu;
    - kuvaa mavazi yasiyo ya heshima;
    - kogombana.
6. mwanafunzi anapaswa kuitika mara moja na kukimbilia alikoitwa;
7. mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi, nembo ya taifa, wimbo wa taifa na fedha za taifa;
8. mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula na ofisi za shule;
9. mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia njema mahali popote alipo;
10. mwanafunzi anatakiwa kunyoosha mkono na kusimama anapouliza/kujibu swali;
11. mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya muda wote anapokuwa darasani, asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.

1.1: MAHUDHURIO.

1. mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shuleni kwa muda wote wa mihula ya masomo;
2. mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

1.2: SHERIA ZA SHULE.

1. uvaaji wa sare za shule ni wa lazima kwa kila mwanafunzi wakati wote:-
    - mwanafunzi anapokwenda hospitalini/ibadani n.k
    - maandamano;
    - mwanafunzi anaposafiri kuja shule au anaporudi nyumbani.

2. mwanafunzi anatakiwa kuwa na kibali/fomu ya ruhusa anaposafiri nje ya mipaka ya shule na akionyeshe kinapohitajika;
3. mwanafunzi anatakiwa kuwa na vazi la kazi(shamba dress) wakati wa kazi za mikono;
4. mwanafunzi anatakiwa kuwa na nguo z michezo na azitumie wakati wa michezo tu;
5. kofia, kiatu chenye kisigino kirefu na mapambo ya aina yoyote hakitakiwi shuleni;
6. usafi wa sare za shule na mavazi yote yaliyoruhusiwa ni wa lazima.

1.3: mipaka ya shule.

1. mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule ila kwa kibali maalumu;
2. mwanafunzi atatoka njje ya mkipaka ya shule kwa pasi maalumu ya kutolea ruhusa ya kutoka nje ya mipaka ya shule;
3. mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:
    - nyumba za walimu na watumishi wasio walimu;
    - ofisi ya walimu ila kwa ruhusa/sababu maalumu;
    - maabara;
    - jikoni;
    - vilabu vya pombe;
    - majumba ya starehe;
    - nyumba zakufikia wageni (guest house).

MUHIMU:

usafi wa mwili na mazingira yote yanayozunguka shule nilazima kwa mwanafunzi wa oldonyo lengai sekondari. hii ni sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku.anatakiwa kuweka viwanja katika hali ya usafi na ya kuvutia wakati wote. takataka zote zitupwe kwenye mashimo ta taka na kuchomwa mara moja. fuata njia zilizopo shuleni kwenda unakoelekea kila wakati na usikatize pasipo na njia.

1.4: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. wizi wa aina yoyote;
2. uasherati, ubakaji na ushoga;
3. ulevi na matumizi ya dawa za kulevya;
4. uvutaji bangi;
5. makosa ya jinai;
6. kupigana au kupiga;
7. kuharibu mali ya shule kwa makusudi;
8. kudharau bendera ya taifa;
9. kuoa au kuolewa;
10. kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule;
11. kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo shuleni;
12. kukataa kwa makusudi adhabu ya mkuu wa shule;
13. kutoa mimba;
14. kutohudhuria vipindi darasani kwa Muda wa siku 90+;
15. kuvuruga amani na usalama wa watu wengine shuleni;
16. kukataa kutii amri halali ya mwalimu, kiranja au mtumishi asiye mwalimu;
17. kumiliki simu,laini,kasha ya simu,santuri za muziki,flashi,betri,chaja,memori kadi,kifaa chochote na kifaa chochote kitumiacho umeme.

Kwa mawasiliano zaidi piga namba zifuatazo:

Mkuu wa shule 0784758601/0735758601 **AU** 0762467528 **makamu**.

SHULE YA SEKONDARI OLDONYO LENGAI

Namba za mwalimu wa darasa (kidato cha kwanza) ni 0714 777 991

A. TAARIFA ZA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI

Naahidi kukubali kushirikiana na shule kumlea mwanafunzi

1. Jina kamili .....
2. Umri .....
3. Kazi yake: .....
4. Anwani ya nyumbani: .....
5. Kijiji ..... Kata ..... Tarafa .....M M.....

   Wilaya ..... Mkoa .....

6. Dini ya mlezi/mzazi ..... Namba ya simu .....
7. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe .....
8. Anwani kamili ya nyumbani ambapo unataka mwanao aende wakati wa likizo .....Simu .....
9. Anwani ya kazini iwapo inatofautiana na ya nyumbani .....

Nathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa hapo juu ni sahihi na kweli.

Jina la mzazi / mlezi .....

Naahidi wakati wote kumlea na kumtunza mwanangu ili awe na tabia njema siku zote. Nitatimiza mahitaji yake yote kulingana na miongozo ya shule. Juu ya hayo naelewa kuwa mwanafunzi akienda kinyume na sheria za shule za kinidhamu zitachukuliwa hata ikibidi kufukuzwa shule.

B: UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI KUKUBALI KUSOMA SHULE HII NA KUWA MWENYE NIDHAMU NA MTIIFU.

Mimi ..... wa kidato cha kwanza Mwaka 2024 Naahidi mbele ya mzazi / mlezi wangu kuwa :-

I. i. Nitatii amri zote za shule na miongozo itakayotolewa na mkuu wa shule , walimu, wafanyakazi na viongozi wa wanafunzi wenzangu.
II. Nitatimiza wajibu wangu wote ulionileta shuleni.
III. Nitahudhuria masomo darasani na popote nitakapohitajika.
IV. Nitakuwa ndani ya mipaka ya shule wakati wowote nitakapohitajika.

Baada ya kusoma na kuelewa haya yote ikiwa ni pamoja na miongozo , sheria na amri; ninaahidi nikiwa na ufahamu sahihi kuwa nikienda kinyume na sheria za shule nipewe adhabu kali ikibidi nifukuzwe shule.

Tarehe ..... sahihi ya mwanafunzi .....

Tarehe ..... Sahihi ya mzazi/mlezi .....

Tarehe ..... Sahihi ya mkuu wa shule. .....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS

FROM THE HEAD OF SCHOOL
OLDONYOLENGAI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 26, MTO WA MBU,

TO MEDICAL OFFICER,

_____
_____
_____

STUDENT'S NAME_____

Please examine the above named student as to his/her fitness for entering to this school in form I.

1. Stool count (Red and white) _____
2. Urinal analysis _____
3. T.B. Test _____
4. Ear test _____
5. Chest test _____
6. Spleen_____
7. Abdomen _____

****** (check passes if pregnancy for girl) *****

Additional information E.g. Physical defect of Impairments in infection chronic of family, diseases etc.

_____
_____
_____
_____

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by medical officer)
I have examined the above and consider that he/she is physically fit for appointment/ engagement as above.

Date _____ Signature_____

Station: _____ Designation_____
NOTE: To the medical officer at the time for examination. Please treat an individual ailment you note. ***** (delete as necessary).